WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

FIDIA e NEWSLETTER

TOLEO LA JULAI-SEPTEMBA 2026 | www.wcf.go.tz



UTEKELEZAJI WA DIRA YA 2050: WCF YAJENGA MIUNDOMBINU YA NISHATI SAFI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Karibu Sana

WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

YALIYOMO:

1. Utekelezaji wa Dira ya 2050: WCF Yajenga Miundombinu ya Nishati safi katika Shule za Sekondari
2. Idara ya kazi na WCF zaweka Mkakati wa kutoa Elimu kwa Wadau kuhusu Fidia kwa Wafanyakazi na Utekelezaji wa Sheria za Kazi
3. Mgodi wa GGM Wapongezwa kwa Kuzingatia Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi
4. WCF Yathibitisha Uhimilivu na Uendelevu kwa miaka 30 ijayo
5. WCF Yaibuka Kinara Maonesho ya Sabasaba
6. WCF yashiriki C-CEOS Forum 2026, yatoa Msisitizo Ulinzi wa Nguvu kazi

Jarida Mtandaoni
Skani Kodi ya QR
Hapo Chini

TIMU YA WAHARIRI
MWENYEKITI
Dkt. John K. Mduma

MHARIRI MKUU
Laura G. Kunenge

MHARIRI MSAIDIZI
Sophia F. Mtakasimba

WACHANGIAJI
Mcharo S. Mrutu
Meseka Z. Kadala
Lilian R. Shembilu
Nuru A. Mwakivuma

DIBAJI



Ndugu Wasomaji, ni furaha kubwa kuwakaribisha katika toleo la Robo ya Kwanza ya Jarida la Fidia kwa mwaka 2026/2027. Toleo hili linatoa taswira ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), pamoja na jitihada zinazoendelea katika kuhakikisha wafanyakazi, waajiri na wadau wanafahamu na kunufaika na huduma zinazotolewa na Mfuko.

Katika kipindi hiki, WCF imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wadau kuhusu haki, wajibu na taratibu za fidia kwa wafanyakazi. Tunaamini kuwa uelewa sahihi wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ni msingi muhimu wa kulinda nguvu kazi ya Taifa na kuhakikisha wafanyakazi wanaopata ajali, magonjwa au vifo vinavyotokana na kazi wanapata stahiki zao kwa wakati.

WCF pia imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kurejesha kwa jamii kupitia miradi yenye kugusa maisha ya wananchi. Katika kipindi hiki, Mfuko umeunga mkono matumizi ya nishati safi ya kupikia katika shule za Sekondari Kinambeu na Kizaga wilayani Iramba, hatua inayochangia utunzaji wa mazingira, afya na mazingira bora ya kujifunzia kwa wanafunzi.

Aidha, tunajivunia kutambuliwa kwa WCF kwa kuibuka mshindi wa kwanza katika kundi la Hifadhi ya Jamii na Bima katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba). Tuzo hii ni ishara ya kuthamini juhudi za Mfuko katika kutoa elimu, huduma na taarifa kwa umma, na inatupa hamasa zaidi ya kuendelea kuboresha huduma na kuimarisha uhusiano na wadau wetu.

Tunatambua kuwa mafanikio haya yanawezekana kutokana na ushirikiano wa watumishi wa WCF pamoja na wadau wetu mbalimbali. Hivyo, napenda kuwashukuru waajiri, wafanyakazi, Serikali na wadau wote kwa ushirikiano wao katika kutekeleza dhamana ya Mfuko ya kulinda nguvu kazi ya Taifa.

Niwahakikishie kuwa WCF itaendelea kuweka mkazo katika ubora wa huduma, elimu kwa wadau, uwajibikaji na ubunifu, ili kuhakikisha tunatimiza dhamana tuliyopewa kwa ufanisi na kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi. Nawakaribisha kusoma jarida hili na kuendelea kushirikiana nasi katika kujenga mfumo imara na endelevu wa fidia kwa wafanyakazi nchini.

Dkt. John K. Mduma
Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

UTEKELEZAJI WA DIRA YA 2050: WCF YAJENGA MIUNDOMBINU YA NISHATI SAFI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu akizungumza wakati wa kukabidhi Miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika Shule ya Sekondari Kinambeu Wilayani Iramba.

Katika kuunga mkono utekelezaji wa Dira ya 2050 pamoja na kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi nchini, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umejenga miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika shule za sekondari zilizopo wilaya ya Iramba mkoani Singida.

Uwekezaji huo unalenga kuboresha utunzaji wa mazingira pamoja na utoaji wa elimu bora katika maeneo ya pembezoni kwa lengo la kuhakikisha ustawi wa mazingira, usalama wa afya na ustawi wa wanafunzi wanaosoma katika shule hizo kwa kupunguza athari za matumizi ya nishati isiyo safi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu, amebainisha hayo wakati wa hafla ya makabidhiano ya mradi wa miundombinu ya nishati safi katika Shule ya Sekondari Kinambeu iliyopo wilayani humo uliofadhiliwa na WCF kupitia sera yake ya kurejesha kwa jamii ambayo imejielekeza kusaidia katika maeneo ya elimu, afya pamoja na utunzaji wa mazingira.

Mhe. Deus Sangu, alisema kwamba utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya 2050 ambayo pamoja na maeneo mengine inasisitiza umuhimu wa utunzaji wa mazingira, pamoja na kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametambuliwa kama kinara wa utunzaji wa mazingira Barani Afrika.

"Tunapowezesha shule kutumia nishati safi ya kupikia, tunapunguza uwezekano wa wanafunzi, walimu na watumishi kuathiriwa na moshi unaotokana na matumizi ya nishati isiyo safi," alisema Mhe. Sangu na kutoa wito kwa jamii kutozichukulia juhudi hizo kama suala la nishati pekee, bali kama sehemu ya kulinda mazingira na afya za wanafunzi.

Katika hatua nyingine, Waziri Sangu alitoa wito kwa waajiri kote nchini kuzingatia sheria za kazi ikiwemo ya Fidia kwa Wafanyakazi, kwa kujiunga na WCF na kuwasilisha michango sahihi ya Wafanyakazi wao katika Mfuko huo ili kulinda nguvu kazi ya Taifa pale wanapopatwa na madhila kazini.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Mhe. Suleimani Mwenda, pamoja na kuishukuru WCF kwa msaada huo, alishukuru pia juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo imekuwa ikitenga fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya ya Iramba.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, alisema kupitia Sera ya Kurejesha kwa Jamii, Mfuko huo umejikita kusaidia sekta ya elimu hasa katika maeneo ya pembezoni.

“Kwa ujumla, ni kwamba Miundombinu hii, sio tu itahamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia katika shule hizi, lakini pia tunaamini kwamba itakuwa ni kichocheo cha utoaji wa elimu bora na hatimaye kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa shule hizi. Hivyo, nitoe wito kwa wanafunzi, waalimu, wazazi na wakazi wa Iramba kwa ujumla kuitunza miundombinu hii ili iwe endelevu kwa muda mrefu,” alisema Dkt. Mduma.

Mbali na kutoa msaada wa miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika Shule ya Sekondari ya Kinambeu, WCF pia imetoa msaada kama huo katika shule ya sekondari ya Kizaga ambazo kwa ujumla shule zote mbili zinahudumia takribani wanafunzi 2,000.



Waziri Sangu akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Mhe. Suleimani Mwenda (wa nne kutoka kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa (WCF) Dkt. John Mduma (wa nne kutoka kulia) pamoja na baadhi ya watumishi wa WCF walioshiriki hafla hiyo.



Waziri Sangu akifurahia pamoja na wanaafunzi wa Shule ya Sekondari Kinambeu



Waziri Sangu akipata maelezo kuhusu namna mfumo wa nishati safi ulivyosaidia watumishi na wanafunzi wa Kinambeu

IDARA YA KAZI NA WCF ZAWEKA MKAKATI WA KUTOA ELIMU KWA WADAU KUHUSU FIDIA KWA WAFANYAKAZI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA ZA KAZI



Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa kikao kazi cha tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Kazi Jijini Dodoma hivi karibuni.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa kushirikiana na Idara ya Kazi iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano zimepanga kuimarisha ushirikiano katika utoaji wa elimu kwa wadau kuhusiana na masuala ya fidia kwa wafanyakazi.

Maeneo hayo ni pamoja na kujengeana uwezo na uelewa juu ya haki, wajibu na taratibu za madai ya fidia kwa wafanyakazi kwa lengo la kuhakikisha haki stahiki inapatikana kwa wakati kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata ugonjwa unaotokana na kazi zao.

Hayo yamejiri jijini Dodoma wakati wa kikao kazi cha tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Kazi kwa mwaka 2025/26 kilichowakutanisha maafisa kazi wafawidhi kutoka mikoa yote nchini.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao kazi hicho, Kamishna wa Kazi Bi. Susan Mkangwa aliwakumbusha maafisa kazi juu ya wajibu wao katika kuimarisha usimamizi wa sheria ya kazi nchini, kufanya kaguzi zenye tija na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili kuimarisha ustawi wa nguvu kazi ya Taifa.



Kamishna wa Kazi Bi. Susan Mkangwa akizungumza wakati wa kikao kazi cha tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Kazi Jijini Dodoma hivi karibuni.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, pamoja na kuwapongeza maafisa kazi kwa namna wanavyoshirikiana na WCF katika kutoa elimu kwa wadau kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi, aliwataka pia kuongeza mkazo katika elimu ya haki na wajibu wa mwajiri na mfanyakazi katika kuhakikisha sheria ya fidia kwa wafanyakazi inazingatiwa.

“Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba elimu tunayotoa haiishii katika kuwaeleza kwamba WCF inalipa fidia pekee, bali pia kuwaeleza kuhusu mfumo mzima wa haki na wajibu wa mfanyakazi, mwajiri na WCF. Kwa mfano, mwajiri ana wajibu wa kujisajili WCF, kulipa michango kwa wakati, kuwasilisha taarifa zinazohitajika, kutoa taarifa kuhusu ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi, kuwasilisha madai pamoja na vielelezo vinavyohitajika, na kuwaelimisha wafanyakazi kuhusu haki zao za fidia. Na kwa mfanyakazi anatakiwa kutoa taarifa kwa wakati kuhusu ajali au ugonjwa unaotokana na kazi, kushirikiana katika uchunguzi wa kitabibu, pamoja na kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayohusu fidia na usalama mahali pa kazi. Elimu tunayotoa leo inaweza kuwa kinga ya kesho kwa mfanyakazi na familia yake,” alisema Dkt. Mduma.

Ushirikiano wa WCF na Idara ya Kazi ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali inayohitaji wizara na taasisi zake kushirikiana katika utendaji kazi kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kuwahudumia wananchi.



Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma akiwa kwenye picha ya pamoja na naadhi ya washiriki.

MGODI WA GGM WAPONGEZWA KWA KUZINGATIA SHERIA YA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imesema mazingira wezeshi ya uwekezaji yaliyowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita yamewezesha Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGM) kutekeleza kikamilifu sheria za kazi ikiwemo sheria ya fidia kwa wafanyakazi na kulinda ustawi wa wafanyakazi na jamii inayouzunguka mgodi huo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Hawa Mchafu, wakati kamati ilipotembelea kukagua utekelezaji wa Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi katika mgodi huo uliopo Manispaa ya Geita.

Mhe. Mchafu amesema GGM imetekeleza kikamilifu sheria ya WCF, ambapo michango na fidia kwa wafanyakazi zinalipwa kwa wakati, hatua inayoonesha dhamira ya kampuni katika kuleta ustawi wa jamii.

Pia kamati iliutaka mgodi huo Mgodi huo kuzingatia udhibiti endelevu wa vihatarishi kazini ili kulinda afya za wafanyakazi wakiwa kazini na hata baada ya kustaafu.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano), Mhe. Dkt. Evaline Munisi, akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Mhe. Deus Sangu, amesema mgodi umetoa ajira zaidi ya 7,000 ikiwemo za moja kwa moja 2,311 na zisizo za moja kwa moja 4,742 kwa Watanzania.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii Bi Hawa Mchafu pamoja na wajumbe wa kamati hiyo wakiwasili katika Mgodi wa GGM kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria ya fidia.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Mahusiano), Mhe. Dkt. Evaline Munisi kazizungumza wakati wa ziara hiyo

Kuhusu michango ya WCF, Dkt. Munisi ameeleza kuwa katika mwaka 2025/26, kiasi cha Shilingi milioni 784 kilichangwa na wafanyakazi, huku katika robo ya kwanza ya mwaka 2026/27, mgodi umechangia Shilingi milioni 198.

Dkt. Munisi ameongeza kuwa WCF imepokea jumla ya madai 61, na kati yake madai 54 sawa na asilimia 87 yameshashughulikiwa, hatua iliyoleta faraja kwa wafanyakazi waliofikwa na majanga kazini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uendelezaji na Mahusiano wa GGM, Gilbert Mworia, amesema kipaumbele cha kampuni ni kuhakikisha haki na afya za wafanyakazi zinalindwa muda wote, na kuahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote ya Kamati ya Bunge.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii wakijionea shughuli za uchimbaji.

WCF YAIBUKA KINARA MAONESHO YA SABASABA

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeibuka mshindi wa kwanza katika kundi la Hifadhi ya Jamii na Bima katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), na hivyo kuendelea kuonyesha nafasi yake katika utoaji wa elimu na huduma kwa umma.

Tuzo hiyo imetolewa mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Mhe. Daniel Francisco Chapo, katika hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na wadau wa sekta ya biashara.

Tuzo hiyo imekabidhiwa na Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Shariff Ali Shariff, na kupokelewa na Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano kwa Umma wa WCF, Bi. Laura Kunenge, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo.



Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Shariff Ali Shariff akimkabidhi Tuzo Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano kwa Umma wa WCF, Bi. Laura Kunenge

Ushindi huo unaonyesha utambuzi wa juhudi za WCF katika kushiriki maonesho hayo kwa kutoa elimu na taarifa kuhusu huduma za Mfuko, hususan masuala ya fidia kwa wafanyakazi, wajibu wa waajiri na haki za wafanyakazi. Kupitia maonesho hayo, WCF imepata fursa ya kuwafikia wadau mbalimbali na kujibu maswali yao kuhusu huduma zinazotolewa na Mfuko.



Aidha, tuzo hiyo ni ishara ya kutambua ubora wa WCF katika kuwasilisha huduma na shughuli zake kwa umma, pamoja na juhudi za kuimarisha uhusiano na wadau. Ushindi huo unaipa WCF hamasa ya kuendelea kuboresha namna inavyotoa elimu na huduma kwa wananchi na wadau wake.

Kwa WCF, tuzo hiyo ina umuhimu wa kipekee kwa kuwa inaongeza utambuzi wa taasisi miongoni mwa wadau wa hifadhi ya jamii na bima, huku ikiakisi dhamira ya Mfuko ya kuhakikisha umma unaelewa huduma zake na namna ya kunufaika nazo. Pia, ni kichocheo kwa WCF kuendelea kutumia majukwaa ya maonesho ya kitaifa kama fursa ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

Maonesho ya Sabasaba ni miongoni mwa majukwaa muhimu yanayowawezesha taasisi za Serikali na sekta binafsi kuwasilisha huduma, bidhaa na fursa mbalimbali kwa umma. Ushindi wa WCF katika maonesho hayo unaongeza nafasi ya Mfuko katika kuendelea kushirikiana na wadau na kujenga uelewa mpana kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi nchini.





WCF YATHIBITISHA UHIMILIVU NA UENDELEVU KWA MIAKA 30 IJAYO



Mkurugenzi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, WCF, Dkt. John Mduma akizungumza wakati wa kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu tathmini ya uhimilivu na uendelevu wa WCF jijini Dodoma

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) una uwezo wa kifedha wa kuendelea kutoa huduma za fidia kwa kipindi cha miaka 30 ijayo. Hayo yamebainika kupitia matokeo ya Tathmini ya Tatu ya Kihesabu ya Mfuko (Actuarial Valuation) iliyofanywa na kampuni ya Kenbright Actuarial and Financial Services.

Tathmini hiyo ni takwa la kisheria linalolenga kutathmini hali ya kifedha ya Mfuko, uwezo wake wa kutimiza wajibu wa kulipa fidia kwa wanufaika pamoja na kuhakikisha uendelevu wa huduma zake kwa muda mrefu.

Matokeo hayo yaliwasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha wadau kilicholenga kupata maoni na mapendekezo yatakayosaidia kuimarisha uendelevu wa Mfuko na kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau wake.

Katika kikao hicho, wadau walisisitiza umuhimu wa kuimarisha ukusanyaji wa michango, kuongeza jitihada za kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma na haki za wanufaika wa WCF, pamoja na kupanua wigo wa huduma za Mfuko ili kuwafikia wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi.

Kikao hicho kilihudhuriwa na wawakilishi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano (PMO-LER), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Ofisi ya Msajili wa Hazina (OTR), pamoja na Menejimenti na watumishi wa WCF.

MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU TATHMINI YA UHIMILIVU NA UENDELEVU WA WCF















WCF YASHIRIKI C-CEOS FORUM 2026, YATOA MSISITIZO ULINZI WA NGUVU KAZI



Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Bi. Renatha Rugarabamu akiwa na miongoni mwa washiriki wa C-CEO Forum.

Viongozi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wameshiriki katika Kikao Kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma (C-CEOs Forum) 2026, kilichofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), jijini Arusha, kuanzia tarehe 28 hadi 30 Septemba 2026.

Forum hiyo iliandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na kuwakutanisha Wenyeviti wa Bodi, Watendaji Wakuu na viongozi mbalimbali wa taasisi na mashirika ya umma, pamoja na wadau kutoka sekta binafsi, maendeleo na uwekezaji.

Ikiwa na kaulimbiu Taasisi za Umma zenye Utendaji wa Juu kwa Uchumi Shindani, Jumuishi na Imara: Kuendeleza Dira ya Taifa 2050.” ilitoa fursa kwa viongozi kujadili masuala ya utendaji, utawala bora, matumizi bora ya rasilimali, ubunifu, ushindani na namna taasisi za umma zinavyoweza kuongeza mchango wake katika maendeleo ya Taifa.



Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt.John Mduma akitoa elimu ya fidia kwa mmoja ya washiriki waliotembelea katika banda la maonyesho ya WCF.



Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt.John Mduma akifuatilia mada wakati wa C-CEO Forum



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Dkt. Irene Isaka akisaini kitabu cha wageni katika banda la WCF

Akiwa katika forum hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John K. Mduma, alieleza kuwa WCF inaendelea kutekeleza dhima yake katika kuunga mkono utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050 kwa kuimarisha ulinzi wa nguvu kazi nchini. Alisema WCF ina-hakikisha wafanyakazi wanaopata madhara yatokanayo na ajali au magonjwa yan-ayohusiana na kazi wanapata stahiki zao za fidia na huduma kwa wakati, hatua inayolenga kupunguza athari za madhara ya kikazi na kuhakikisha nguvu kazi ya Taifa inalindwa na kuendelea kuwa na mchango katika maendeleo ya nchi.





Baadhi ya washiriki wakipata elimu ya fidia katika banda la WCF

TANGAZO

TARATIBU ZA KUWASILISHA MADAI

(Kwa Mujibu wa Kifungu cha 77 - Employee Rights Notice)

Kulingana na matakwa ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 [marejeo ya mwaka 2015], mfanyakazi anayo haki ya kupata fidia endapo atapata ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi.



1.0 AJALI

Ajali inamaanisha ajali inayotokana na kazi na kumpelekea mwajiriwa kupata majeraha.
Ajali zinazoshughulikiwa chini ya Sheria ya WCF ni zile zinazotokea katika eneo la mwajiri wakati mfanyakazi akitimiza majukumu yake ya kazi.
Ajali zinazotokea barabarani zinazohusisha chombo cha moto wakati mfanyakazi akiwa njiani anarudi/ anaenda kazini na mfanyakazi akiwa katika kazi maalumu na ajali zinazotokea barabarani zisizohusisha chombo cha moto wakati mfanyakazi akiwa njiani anarudi/ anaenda kazini na mfanyakazi akiwa katika kazi maalumu.

2.0 UGONJWA

Ugonjwa unamaanisha magonjwa yaliyotajwa kwenye jedwali la tatu katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura ya 263] au ugonjwa wowote uliotokana na kazi.

3.0 KIFO

Kifo kitakachosababishwa na ajali kazini au ugonjwa unaotokana na kazi.

4.0 HAKI YA MATIBABU

Mfanyakazi aliyepata ajali inayotokana na kazi anastahili kupatiwa huduma ya matibabu moja kwa moja chini ya utaratibu wa WCF. Huduma ya matibabu inahusisha uchunguzi, dawa, huduma za kitabibu na rufaa ya matibabu pale inapohitajika. Aidha, WCF itatoa kibali cha matibabu ya Ugonjwa baada ya kujiridhisha kama ugonjwa ulioripotiwa unatokana na kazi.

5.0 HAKI YA FIDIA

Mfanyakazi atakayepata ajali au ugonjwa unaotokana na kazi anastahili fidia zifuatazo;

a) Ulemavu wa Muda.
b) Ulemavu wa kudumu na kupoteza uwezo wa kufanya kazi kwa kiwango kilichothibitishwa kitabibu.
c) Huduma ya Utengemao kwa lengo la kumsaidia kuweza kurudi kazini haraka na kushiriki katika shughuli nyingine za kijamii ambazo zitamuingizia kipato na
d) Malipo kwa anayemhudumia mgonjwa ambaye amepata ulemavu wa kudumu unaomfanya ashindwe kufanya shughuli za kijami.

6.0 MAFAO ENDAPO KIFO KITATOKEA

Iwapo mfanyakazi atafariki kutokana na ajali au ugonjwa unaotokana na kazi: Malipo hutolewa kwa mjane, mgane au watoto wa mfanyakazi atakayefariki kutokana na ajali au ugonjwa uliotokana na kazi. Endapo hakuna mjane, mgane au watoto, malipo yatalipwa kwa ndugu wengine wa marehemu watakaotambulika na Mahakama.

"Fidia Stahiki kwa Wakati"

7.0 UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA AJALI, UGONJWA/KIFO

a) Mfanyakazi au mtu yeyote kwa niaba ya mfanyakazi aliyepata ajali/kifo au ugonjwa unaotokana na kazi, ana wajibu wa kutoa taarifa kwenye Ofisi za Utawala, Mratibu wa Usalama Mahala pa Kazi (OHS) au Ofisi za WCF ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi tokea madhila yalipotokea.

14 SIKU

b) Mwajiri atalazimika kuwasilisha taarifa za ajali au ugonjwa unaotokana na kazi kwa njia ya kielektroniki kupitia portal.wcf.go.tz ndani ya siku saba (07) tokea tukio lilipotokea. Aidha, madai ya ajali, ugonjwa au kifo kinachotokana na kazi yanapaswa kuripotiwa WCF ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili (12). Endapo mwajiri au mfanyakazi aliyepata madhila atachelewa kuwasilisha madai kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12) atapoteza vigezo vya kulipwa fidia chini ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263 [marejeo ya mwaka 2015].

12 MIEZI

8.0 UWASILISHAJI WA NYARAKA

a) Mwajiri atalazimika kuwasilisha nyaraka zifuatazo kupitia *portal.wcf.go.tz*

AJALI

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya tukio la ajali kazini.
c) Fomu ya Madai (WCC 1).
d) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

UGONJWA

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya uchunguzi kutoka kwa Daktari.
c) Fomu ya Madai (WCC 1).
d) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

KIFO

a) Nakala ya Mkataba wa kazi au barua ya ajira.
b) Ripoti ya tukio la ajali kazini.
c) Nakala ya Cheti cha Kifo.
d) Nakala ya Kibali cha Mazishi.
e) Fomu ya Madai (WCC 1).
f) Ripoti ya Polisi ikiwa ajali imetokea nje ya eneo la kazi ikihusisha chombo cha moto au jinai.

b) WCF itamtaarifu mwajiri na mfanyakazi kuhusu kukubaliwa au kukataliwa kwa taarifa ya tukio la ajali, ugonjwa au kifo baada ya uhakiki.

c) Mwajiriwa ambaye taarifa yake ya tukio la ajali imekubalika ataendelea na hatua ya uwasilishaji wa fomu za matibabu au nyaraka za mirathi:

FOMU ZA WCF ZA MATIBABU (mgonjwa anayeendelea na matibabu)

a) Ripoti ya awali ya matibabu (WCC-2A).
b) Ripoti ya maendeleo ya matibabu (WCP – 3) – Ijazwe kila mgonjwa anapoenda kliniki.
c) Taarifa za Mfanyakazi za Kibenki.

FOMU ZA WCF ZA MATIBABU (mgonjwa anayeendelea na matibabu)

a) Ripoti ya awali ya matibabu (WCC-2A).
b) Ripoti ya maendeleo ya matibabu (WCP – 3).
c) Ripoti ya Mwisho ya matibabu (WCC-2B).
d) Taarifa za Mfanyakazi za Kibenki.

NYARAKA MIRATHI

a) Kiapo cha Msimamizi wa Mirathi.
b) Hukumu ya Mahakama.
c) Nakala ya Muhtasari wa Kikao cha Familia.
d) Nakala ya Cheti cha Ndoa (kama kuna mjane/mgane).
e) Nakala ya Vyeti vya Watoto (kama kuna watoto).
f) Fomu ya Wategemezi (WCP 7).
g) Taarifa za benki za wategemezi.

9.0 USHUGHULIKIAJI WA MADAI WCF NA KUPATA UFAFANUZI

WCF itashughulikia madai yatakayowasilishwa na kukamilika nyaraka zote zinazohitajika ndani ya siku 30 na kutoa majibu kwa njia ya barua kwa mwajiri na mfanyakazi ya namna fidia ilivyokokotolewa kwa kulipwa. Barua zote zitakazotolewa na WCF zitapatikana katika mfumo wa portal.wcf.go.tz. WCF ina wajibu wa kutoa ufafanuzi wa madai yatakayowasiishwa pale itakapohitajika.

10.0 KINGA DHIDI YA UNYANYASAJI

Mfanyakazi hatakiwi kutishwa, kubughudhiwa, kuadhibiwa au kubaguliwa kwa sababu ya kudai au kutaka kudai fidia. WCF.

"Fidia Stahiki kwa wakati"

HABARI KATIKA PICHA















WCF

Workers Compensation Fund

ISO 9001 : 2015 CERTIFIED

Jarida hili limeandaliwa na
Kitengo cha Uhusiano kwa Umma:
MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF)
Jengo la Kambarage, Ghorofa ya 3,
S.L.P 329, 41104 Dodoma,
TANZANIA